# KANUNI ZA MAADILI YA UTALII DUNIANI

## DIBAJI

**Sisi, Wanachama wa Shirika la Utalii Duniani, tuliokusanyika kwenye Mkutano Mkuu unaofanyika Santiago, Chile leo tarehe 1 Oktoba, 1999,**

**Kwa kusisitiza** madhumuni yaliyowekwa kwenye Ibara ya 3 ya Sheria za Shirika la Utalii Duniani, na kuelewa dhima "muhimu na dhahiri" ya shirika hili, kama inavyotambuliwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, katika kukuza na kuendeleza utalii kwa lengo la kuchangia katika maendeleo ya uchumi, maelewano ya kimataifa, amani, ustawi na heshima ya kimataifa na kufuata haki za binadamu na uhuru wa msing kwa wote bila ubaguzi wa rangi, jinsia, lugha au dini,

**Kwa kuamini kwa dhati** kwamba, kupitia mawasiliano ya moja kwa moja ya hiari na yasiyo na mapatano, yanayofanywa kati ya wanaume na wanawake wenye tamaduni na mitindo mbalimbali ya maisha, utalii unawakilisha nguvu muhimu ya amani na kipengele cha urafiki na maelewano miongoni mwa watu ulimwenguni,

**Kwa makubaliano** na mantiki ya kuoanisha uhifadhi wa mazingira, maendeleo ya kiuchumi na vita dhidi ya umaskini kwa hali endelevu, kama ilivyotungwa na Umoja wa Mataifa, katika "Mkutano wa Mazingira" uliofanyika Rio de Janeiro mwaka 1992 na kuelezwa katika Ajenda 21 iliyokubalika kwenye mkutano huo,

**Kwa kuzingatia** kuendelea kukua kwa haraka kwa shughuli za utalii, iwe kwa kujiburudisha, biashara, utamaduni, dini au madhumuni ya kiafya, na athari zake nzuri au mbaya kwa mazingira, uchumi na jamii zinazotoa watalii na kupokea watalii, jamii za wenyeji pamoja na uhusiano wa kimataifa na kibiashara,

**Kwa kukusudia** kukuza utalii unaowajibika, endelevu na unaokubalika kimataifa, katika mazingira ya haki ya watu wote kutumia muda wao wa mapumziko kwa shughuli za burudani au kusafiri kwa kuzingatia matakwa ya jamii ya watu wote,

**Lakini kuridhika** kwamba, tasnia ya utalii duniani kwa ujumla ina nafasi kubwa ya kunufaika kutokana na kuendeshwa katika mazingira yanayojali uchumi wa soko, shughuli za sekta binafsi, biashara huru na yenye lengo la kutumia ipasavyo mafanikio yake katika kuleta ajira na kipato,

**Aidha, kuridhika kwa dhati** kuwa, ikiwa kanuni na sheria zinafuatwa, utalii unaowajibika na endelevu kwa vyovyote vile haupingani na mfumo wa biashara huria ambao unatawala shughuli za biashara ya utoaji huduma katika sekta hii. Hivyo, inawezekana kuoanisha uchumi na ikolojia, mazingira na maendeleo, kukuza biashara ya kimataifa na wakati huohuo kulinda utambulisho wa jamii na utamaduni,

**Kwa kuzingatia kwamba,** kwa mtazamo huo, wadau wote katika uendelezaji utalii, kitaifa, kikanda na katika serikali za vijiji, shughuli za biashara, vyama vya biashara, wafanyakazi katika sekta, Asasi Zisizo za Serikali (AZISE) na bodi zote zilizoko chini ya tasnia ya utalii, pamoja na jamii mbalimbali za wenyeji, vyombo vya habari na watalii wenyewe, wana majukumu mbalimbali yanayotegemeana katika maendeleo ya utalii kibinafsi na kijamii, na kwamba uanzishaji au uundaji wa haki binafsi na kazi zao utasaidia katika kufikia lengo hili,

**Kwa kudhamiria,** kuyakubali madhumuni yaliyohimizwa na WTO tangu kupitishwa kwa Azimio 364 (XII) katika Mkutano Mkuu wa mwaka 1997 (Istanbul) ambayo ni kukuza ubia wa kweli kati ya wadau wa serikali na binafsi katika kuendeleza utalii, na kutaraji kuona ushirikiano wa aina hiyo unakuzwa kwa uwazi na uwiano mzuri, kwa kuwa na uhusiano kati ya nchi zinazotoa, na zinazopokea watalii na shughuli zao za utalii zinazohusika,

**Kwa kufuatilia** maazimio ya Manila ya mwaka 1980 kuhusu utalii duniani na ya 1997 kuhusu athari za kijamii zinazotokana na utalii, pamoja na kuhusu Sheria ya Haki za Utalii na Kanuni za Mtalii zilizopitishwa Sofia mwaka 1985 chini ya usimamizi wa WTO,

**Lakini kwa kuamini** kwamba, vyombo hivi havina budi kujalizwa na seti ya kanuni zinazotegemeana kwa ajili ya ufafanuzi wake na matumizi, ambapo wadau wa maendeleo ya

utalii hawana budi kurekebisha tabia zao mwanzoni mwa karne ya ishirini na moja,

**Kwa kutumia kwa** madhumuni ya chombo hiki, fasili na uainishaji unaofaa kwa safari za kitalii, hususan dhana ya "Mgeni" "Mtalii" na "Utalii", kama zilivyopitishwa na Mkutano wa Kimataifa wa Ottawa, uliofanyika kuanzia Juni 24 hadi 28, 1991 na kuthibitishwa mwaka 1993 na Tume ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa katika mkutano wake wa ishirini na saba,

**Kurejea** hususan kwenye vyombo vifuatavyo:

- Tamko la Haki za Binadamu Duniani la tarehe 10 Desemba 1948;
- Mkutano wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa tarehe 16 Desemba, 1966 ;
- Mkutano wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa wa tarehe 16 Desemba, 1966 ;
- Makubaliano ya Warsaw kuhusu Usafiri wa Anga ya tarehe 12 Oktoba 1929 ;
- Makubaliano ya Chicago kuhusu Usalama wa Anga wa Kimataifa ya Desemba 7, 1944 na Makubaliano ya Tokyo, 'The Hague na Montreal' kuhusiana na maudhui hayo ;
- Makubaliano kuhusu Fursa za Forodha kwa ajili ya Utalii ya tarehe 4 Julai 1954 na Makubaliano yanayohusiana nayo;
- Makubaliano kuhusu Ulinzi wa Urithi wa Utamaduni na Maumbile Asilia Duniani ya tarehe 23 Novemba, 1972 ;
- Azimio la Manila kuhusu Utalii Duniani la tarehe 10 Oktoba, 1980 ;
- Azimio la Mkutano Mkuu wa Sita wa WTO (Sofia) kupitisha Sheria ya Haki za Utalii na Kanuni za Utalii la tarehe 26 Septemba, 1985 ;
- Makubaliano kuhusu Haki za Mtoto ya tarehe 26 Januari, 1990;
- Azimio la Mkutano Mkuu wa Tisa wa WTO (Buenos Aires) hususan uwezeshaji wa safari, usalama na ulinzi wa watalii la tarehe 4 Oktoba, 1991;
- Azimio la Rio kuhusu Mazingira na Maendeleo la tarehe 23 Juni, 1992;
- Makubaliano ya jumla kuhusu biashara za huduma ya tarehe 15 Aprili, 1994;
- Makubaliano kuhusu Bioanuwai ya tarehe 6 Januari, 1995;
- Azimio la Mkutano Mkuu wa Kumi na Moja wa WTO (Cairo) kuhusu kuzuia biashara ya utalii wa ukahaba la tarehe 22 Oktoba, 1995;

- Azimio la Stockholm la tarehe 28 Agosti, 1996 dhidi ya Biashara ya Ngono shurutishi kwa Watoto;
- Azimio la Manila kuhusu Athari za Utalii kwa Jamii la tarehe 22 Mei, 1997;
- Makubaliano na mapendekezo yaliyopitishwa na Shirika la Kazi Duniani katika eneo la makubaliano ya pamoja ya ukomeshaji wa kazi za kitumwa, ajira kwa watoto, utetezi wa haki za wazawa, kuwatendea sawa na kutokuwa na ubaguzi mahali pa kazi ;

**Tunakubali kuwepo kwa haki ya utalii na uhuru wa kufanya safari za kitalii**

**tunatamka nia yetu ya kukuza utaratibu wa utalii duniani wa usawa, unaowajibika na endelevu, ambao manufaa yake yatagawiwa kwenye sekta zote za jamii katika hali ya uchumi wa kimataifa wa wazi na huru, na**

**kwa pamoja tunapitisha Kanuni za Sheria ya Maadili ya Utalii Duniani, ili kutimiza malengo hayo.**

## *Ibara ya 1*

Mchango wa utalii kwa uelewano wa pamoja na heshima kati ya watu na jamii mbalimbali,

1. Uelewa na ukuzaji wa maadili ya utu, tabia ya uvumilivu na kuheshimu tofauti za dini, imani za kifalsafa na za kiroho, vyote hivi ni msingi na matokeo ya utalii unaowajibika; wadau katika maendeleo ya utalii na watalii wenyewe hawana budi kuzingatia mila za kijamii na kiutamaduni na tabia za watu wote, wakiwemo makabila madogo, wazawa pamoja na kutambua thamani yao;

2. Shughuli za utalii hazina budi kuendeshwa bila kuathiri sifa na mila za kanda na nchi mwenyeji, kwa kuheshimu sheria, tabia na desturi zao ;

3. Jamii za wenyeji kwa upande mmoja na wataalamu wenyeji kwa upande mwingine, hawana budi kuwazoea na kuwaheshimu watalii wanaowatembelea na kujifunza kuhusu maisha yao, aidha, kuhakikisha kwamba, elimu na mafunzo waliyopata wataalamu, vinachangia kwenye makaribisho ya ukarimu,

4. Ni jukumu la Mamlaka za Umma kutoa ulinzi kwa watalii na wageni na mali zao; hazina budi pia, kuzingatia usalama wa watalii wa nje, kwa kuwa wao ni rahisi zaidi kudhuriwa; Mamlaka hizi hazina budi kuwezesha uanzishwaji wa njia mahususi za upashanaji habari, uimarishaji ulinzi na usalama, utoaji bima na msaada unaoendana na mahitaji yao ; vitendo vya mashambulizi , uvamizi, utekwaji nyara au vitisho dhidi ya watalii au wafanyakazi wa tasnia ya utalii ; pamoja na uharibifu wa makusudi wa nyezo za utalii au za vipengele vya urithi wa kiutamaduni au maumbile asilia havina budi kulaaniwa vikali na wahusika kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria za nchi zao ;
5. Watalii na wageni wanaposafiri wasifanye kosa lolote la jinai au kitendo chochote

kinachohesabiwa kuwa cha jinai kwa mujibu wa sheria za nchi waliyotembelea na waepuke tabia yoyote inayoonekana kuwa na madhara au uharibifu kwa wenyeji, au yenye uwezekano wa kuharibu mazingira ya nchi; hawana budi kuepuka usafirishaji wa dawa haramu za kulevya, silaha, zana za kale, spishi zinazolindwa, mazao na vitu ambavyo ni hatari au vilivyopigwa marufuku au kukatazwa kwa mujibu wa kanuni za nchi;

6. Kabla ya kuondoka nchini kwao, watalii na wageni wana jukumu la kujifunza mambo ya nchi wanayojiandaa kutembelea, hawana budi kuelewa hatari za kiafya na kiusalama kwa safari yoyote nje ya mazingira yao ya kawaida na kuwa na tabia itakayowafanya wapunguze hatari hizo;

## *Ibara ya* 2

Utalii kama chombo cha kujiridhisha binafsi au kwa pamoja

1. Utalii, shughuli ambayo mara nyingi inahusishwa na mapumziko na burudani, michezo na fursa ya kuona utamaduni na maumbile asilia, hauna budi kupangwa na kutekelezwa kama njia bora ya kujiridhisha mtu binafsi au kundi; iwapo unafanywa kwa nia njema, ni kipengele kisicho na mbadala cha kujielimisha, kuvumiliana na kwa kutoa mafunzo kuhusu tofauti halisi kati ya watu na tamaduni mbalimbali;

2. Shughuli za utalii hazina budi kuheshimu usawa wa wanawake na wanaume, kukuza haki za binadamu hususan haki za kila mtu na makundi yaliyo hatarini zaidi kuathirika, hasa watoto, wazee, walemavu, makabila madogo madogo na wazawa;

3. Unyonyaji wa binadamu wa aina yoyote, hasa wa ngono, unapotumiwa kwa watoto, hupingana na madhumuni ya msingi ya utalii na ni kinyume cha utalii;

kwa hali hiyo, kwa mujibu wa Sheria ya Kimataifa, unapaswa kupigwa vita kwa nguvu zote, kwa ushirikiano wa nchi zinazohusika na kuadhibiwa bila huruma kwa sheria za nchi zote mbili yaani sheria za nchi inayotembelewa na nchi anakotoka mgeni, hata kama hukumu zinatolewa nchi za nje;

4. Safari kwa madhumuni ya kidini, kiafya, kielimu na ubadilishanaji wa utamaduni, na utaalamu wa lugha ni aina za utalii zenye manufaa, zinazostahili kuhimizwa;

5. Uingizwaji kwenye mitaala ya shule elimu kuhusu utalii, manufaa yake kijamii, kiuchumi, kiutamaduni pamoja na hatari zake hauna budi kuhimizwa ;

## *Ibara ya 3*

Utalii, kipengele cha maendeleo endelevu

1. Wadau wote wa uendelezaji utalii hawana budi kulinda mazingira ya asili kwa lengo la kukuza uchumi imara na endelevu, unaolenga kutosheleza kwa usawa mahitaji na matarajio ya kizazi cha sasa na kijacho;

2. Aina zote za uendelezaji utalii unaofaa kulinda rasilimali adimu na za thamani kubwa, hasa maji na nishati, na ambazo zinaepuka kwa kiwango kikubwa uzalishaji taka, hazina budi kupewa kipaumbele na kuhimizwa na mamlaka za kitaifa, kimkoa na Serikali za Mitaa;

3. Kuyumbayumba kwa wakati na muda wa mtiririko wa watalii na wageni, hasa wale wanaotokana na likizo iliyolipwa, likizo za shule, hivyo likizo zilizosambazwa vizuri hazina budi kutafutwa ili kupunguza shinikizo linaloletwa na shughuli za utalii kwa mazingira na kuongeza faida kwa tasnia ya utalii na uchumi wa eneo husika;

4. Miundombinu ya utalii haina budi kubuniwa na shughuli za utalii kupangwa ili

kuweza kulinda urithi wa maumbile asilia wenye mifumoikolojia na bioanuwai na kuhifadhi spishi za wanyamapori zilizo hatarini kutoweka; wadau wa uendelezaji utalii, na hasa wataalamu, hawana budi kukubaliana na kuwekwa kwa masharti katika shughuli zao wakati zinapofanywa katika maeneo ambayo ni nyeti hasa: jangwani, ncha za dunia au maeneo ya milima mirefu, maeneo ya mwambao, misitu ya tropiki au maeneo chepechepe, yanayofaa kuanzishia hifadhi ya viumbe au maeneo yaliyohifadhiwa;

5. Utalii wa maumbile asilia na utalii unaojali mazingira hutambuliwa kuwa vinafaa zaidi kwa kustawisha na kuimarisha hali ya utalii, alimradi vinaheshimu urithi wa kimaumbile na watu wa eneo husika kulingana na uwezo wa kustahimili wa eneo hilo.

## *Ibara ya 4*

Utalii, mtumiaji wa urithi wa utamaduni wa binadamu na mchangiaji wa uimarishaji wake

1. Rasilimali za utalii ni mali ya urithi wa pamoja wa binadamu, hivyo jamii zilizo katika maeneo hayo zina haki mahususi na wajibu kwa rasilimali hizo;

2. Sera na shughuli za utalii hazina budi kufanywa kwa kuthamini urithi wa kisanii, kiakiolojia na kiutamaduni, ambazo hazina budi kulindwa na kurithishwa kwa vizazi vijavyo; utunzaji mahususi hauna budi kufanywa katika kuhifadhi na kuinua viwango vya minara ya kihistoria, maeneo ya ibada na makumbusho pamoja na maeneo ya kiakiolojia na ya kihistoria ambayo hayana budi kufunguliwa zaidi kwa ziara za watalii; iwepo fursa kwa umma kutembelea mali za kiutamaduni na minara ya historia inayomilikiwa binafsi na kuheshimu haki za wamiliki wake, pamoja na majengo ya kidini, bila kuathiri mahitaji ya kawaida ya wanaoabudu;.

3. Mapato yatokanayo na ziara kwenye maeneo ya kiutamaduni na minara ya kihistoria, hayana budi, angalau kwa kiasi fulani, kutumiwa kwa ajili ya utunzaji, uendeshaji, maendeleo na ukarabati wa maeneo ya urithi huo;

4. Shughuli za utalii hazina budi kupangwa kwa namna ambayo zitaruhusu bidhaa za utamaduni za maeneo husika, sanaa za mikono na sanaa za jadi kudumishwa na kustawi, kuliko kusababisha kusawijika na kuondoa uasili wake ;

## *Ibara ya 5*

Utalii, shughuli yenye manufaa kwa nchi wenyeji na jamii

1. Wenyeji wa maeneo hayo hawana budi kuhusishwa na shughuli za utalii na kugawana kwa usawa manufaa ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni waliyozalisha na hasa katika kuanzisha ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja zinazotokana na utalii;

2. Sera za utalii hazina budi kutumiwa katika njia ambayo itasaidia kuinua kiwango cha maisha ya watu wa maeneo yaliyotembelewa na kukidhi mahitaji yao; upangaji na usanifu wa majengo na uendeshaji wa maeneo ya starehe na malazi havina budi kuunganishwa kadri iwezekanavyo; katika mfumo wa uchumi na jamii, pale ambapo ujuzi ni sawa, kipaumbele hakina budi kutolewa kwa watumishi wenyeji;

3. Mkazo maalumu hauna budi kuwekwa katika matatizo mahususi ya maeneo ya mwambao na visiwani na kwa maeneo ya vijijini na maeneo ya milimani yaliyo hatarini, ambayo mara nyingi utalii unawakilisha fursa adimu kwa ajili ya maendeleo katika kipindi cha kuzorota kwa shughuli za kiuchumi zilizozoeleka;

4. Wataalamu wa utalii, hasa wawekezaji, wakiongozwa na kanuni zilizowekwa na mamlaka ya serikali, hawana budi kufanya utafiti wa athari za miradi yao ya maendeleo katika mazingira na mandhari ya kimaumbile asilia, hawana budi pia kuwasilisha, kwa uwazi zaidi bila kupendelea, taarifa kuhusu mipango yao ya baadaye na athari zake zinazoweza kutokea na kuanzisha mazungumzo kuhusu maudhui ya mipango yao na watu wanaohusika;

## *Ibara ya 6*

Majukumu ya wadau katika uendelezaji utalii

1. Wataalamu wa utalii wana jukumu la kuwapa watalii taarifa sahihi kuhusu maeneo yao ya utalii na hali ya usafiri, ukarimu na makazi; hawana budi pia kuhakikisha kwamba vifungu vya mikataba walivyopendekeza kwa wateja wao vinaeleweka vizuri kuhusu hali, gharama na ubora wa huduma wanazoahidi kutoa na fidia za fedha zitakazolipwa itokeapo ukiukaji wa mkataba kwa makusudi kwa upande wao;

2. Wataalamu wa utalii, kadri wanavyotegemewa, hawana budi kuonyesha kuhusika kwao kwa kushirikiana na mamlaka za serikali, katika masuala ya usalama na ulinzi, tahadhari ya ajali, kinga ya afya na usalama wa chakula kwa wale wanaotumia huduma zao; hali kadhalika, hawana budi kuhakikisha kuwepo kwa mifumo mizuri ya bima na misaada; hawana budi kukubali majukumu ya utoaji taarifa yaliyoelezwa na kanuni za kitaifa na kulipa fidia inayoridhisha endapo watashindwa kwa upande wao kufuata majukumu yao ya mkataba;

3. Wataalamu wa utalii, kwa kuwa suala hili linawategemea wao, hawana budi kuchangia katika uridhishaji wa kiutamaduni na kiroho wa watalii na kuwaruhusu kuendesha ibada wakati wa safari zao;

4. Mamlaka za Serikali za nchi zinazotoa watalii na nchi wenyeji, kwa kushirikiana na wataalamu wanaohusika pamoja na vyama vyao, hawana budi kuhakikisha kwamba upo utaratibu unaotakiwa kwa ajili ya kuwarudisha kwao watalii itokeapo kufilisika kwa kampuni iliyowatayarishia safari zao;

5. Serikali zina haki na jukumu hasa litokeapo tatizo, kuwaarifu raia wao kuhusu hali ngumu, au hata hatari watakazokabiliana nazo wakati wa safari zao nchi za nje; hata hivyo ni jukumu lao kutoa taarifa ya namna hiyo bila upendeleo au katika hali isiyokubalika au kupigwa chuku juu ya tasnia ya utalii ya nchi wenyeji na maslahi ya waendeshaji wake; kwa hiyo maudhui ya washauri wao wa safari hayana budi kujadiliwa kabla na mamlaka ya nchi wenyeji na wataalamu wanaohusika; mapendekezo yatakayotayarishwa hayana budi kulingana na uzito wa hali watakazokutana nazo na yahusu maeneo ya kijiografia ambapo hatari imetokea; ushauri wa aina hiyo hauna budi kurekebishwa au kufutwa mara baada ya usalama kurudi katika hali ya kawaida;

6. Vyombo vya habari, hasa vile vilivyobobea katika habari za safari, zikiwemo njia za kisasa za mawasiliano kwa njia ya elektroniki, havina budi kutoa taarifa za uhakika na zisizo na upendeleo kuhusu matukio na hali zinavyoweza kuathiri mtiririko wa watalii; havina budi pia kutoa taarifa sahihi na za kuaminika kwa watumiaji wa huduma za utalii; tekinolojia mpya za biashara ya elektroniki na mawasiliano haina budi kuendelezwa na kutumiwa kwa madhumuni haya; na kama ilivyo kwa upande wa vyombo vya habari, kwa hali yoyote ile visikuze utalii wa ngono;

## *Ibara ya 7*

Haki ya Kutalii

1. Matarajio ya kwenda moja kwa moja na kwa binafsi kwenye uvumbuzi na burudani katika rasilimali za dunia, ni haki sawa na iliyo wazi kwa wakazi wote duniani na

ushiriki mkubwa unaoongezeka katika utalii wa kitaifa na kimataifa hauna budi kuhesabiwa kama mojawapo ya njia nzuri zinazowezekana kuelezea ukuaji endelevu wa muda wa mapumziko, na kusiwe na vipingamizi mbele yake;

2. Haki ya kutalii kwa wote haina budi kutazamwa kama matokeo ya haki ya kupumzika na kuburudika, ikiwemo ukomo wa saa za kazi unaokubalika na likizo za vipindi zenye malipo kama zilivyotolewa kwenye Ibara ya 24 ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu na Ibara ya 7.d ya Mkutano wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiutamaduni, Kijamii na Kiuchumi;

3. Utalii wa kijamii, na hasa utalii shirikishi, unaotoa fursa pana ya kupata burudani, starehe, safari na mapumziko, hauna budi kuendelezwa kwa msaada wa mamlaka za serikali;

4. Utalii wa familia, vijana, wanafunzi na wazee, na utalii wa watu wenye ulemavu hauna budi kuhimizwa na kuwezeshwa;

## *Ibara ya 8*

Uhuru wa matembezi ya kitalii

1. Watalii na wageni hawana budi kunufaika, kwa mujibu wa Sheria za Kitaifa na Kimataifa, kutokana na uhuru wa kusafiri ndani ya nchi zao na kutoka nchi moja hadi nyingine, kwa mujibu wa Ibara ya 13 ya Azimio la Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu; hawana budi kufikia mahali pa mpito, pa kukaa, na kwenye maeneo ya utalii na ya utamaduni bila ya kulazimika kufuata taratibu nyingi au ubaguzi;

2. Watalii na wageni hawana budi kutumia aina zote za mawasiliano zilizopo ndani na nje ya nchi; hawana budi kunufaika na upatikanaji rahisi na haraka wa huduma za afya, sheria na uongozi wa nchi; hawana budi kuwa huru kuwasiliana na

wawakilishi wa kibalozi wa nchi zao kwa mujibu wa makubaliano ya kibalozi yaliyopo;

3. Watalii na wageni hawana budi kunufaika kwa kuwa na haki sawa na raia wa nchi wanayotembelea kuhusu data na taarifa binafsi za siri zinazowahusu, hasa zilizohifadhiwa kielektroniki;

4. Taratibu za kiutawala kuhusu uvukaji mipaka iwe zilizo katika uwezo wa nchi au zinazotokana na mikataba ya kimataifa, kama vile viza au taratibu za afya na forodha, hazina budi kutumiwa kadri iwezekanavyo, ili kuwezesha uhuru wa kusafiri na kufikia kwa ukamilifu utalii wa kimataifa; makubaliano kati ya vikundi vya nchi kuwianisha na kurahisisha taratibu hizi hayana budi kuhimizwa; kodi mahususi na ushuru vinavyotozwa kwenye tasnia ya utalii na kudhoofisha uwezo wake hazina budi kuondolewa hatua kwa hatua au kusahihishwa;

**5.** Kadri hali ya uchumi ya nchi wanazotoka inavyoruhusu, wasafiri hawana budi kuwa na posho za kujikimu zinazoweza kubadilishika kulingana na mahitaji ya safari zao;

## *Ibara ya 9*

Haki za wafanyakazi na wajasiliamali katika sekta ya utalii

1. Haki za msingi za wafanyakazi wanaolipwa mishahara na wanaojiajiri wenyewe katika tasnia ya utalii na shughuli zinazohusiana nazo, hazina budi kutolewa chini ya usimamizi wa tawala za kitaifa na serikali za vijiji kwenye nchi zao za asili na nchi wenyeji na msisitizo uwekwe, hususan, kwenye matatizo yanayoambatana hasa na mabadiliko ya misimu katika shughuli zao, upana wa tasnia yao duniani, ambao mara nyingi huhitajika kutokana na hali ya kazi yao;

2. Wafanyakazi wanaolipwa mshahara na wanaojiajiri wenyewe katika tasnia ya utalii na shughuli zinazohusiana nazo wana haki na wajibu wa kupata mafunzo ya awali na yenye mwendelezo yanayofaa; hawana budi kupewa ulinzi wa kutosha wa kijamii; kutokuwa na uhakika wa ajira hakuna budi kupunguzwa kadri iwezekanavyo; na hadhi mahususi, kwa kuzingatia ustawi wao kijamii, haina budi kutolewa kwa wafanyakazi wa msimu wa sekta hiyo;

3. Mtu yeyote awe na uraia wa kuzaliwa au wa kisheria, alimradi ana uwezo na ujuzi vinavyotakiwa anastahiki kuendeleza shughuli ya kitaalamu katika uga wa utalii kulingana na sheria za nchi zilizopo, wajasiliamali na wawekezaji hasa katika eneo la kampuni ndogo na za kati wana uhuru wa kuingia katika sekta ya utalii kwa masharti nafuu ya kisheria au ya kiutawala;

4. Fursa za ubadilishanaji wa uzoefu zinazotolewa kwa watendaji na wafanyakazi, wenye mshahara au wasio na mshahara, kutoka nchi mbalimbali, huchangia katika kukuza maendeleo ya utalii dunaini; jitihada hizi hazina budi kuwezeshwa kadri iwezekanavyo kwa mujibu wa sheria za nchi na makubaliano ya kimataifa;

5. Kama kipengele cha mshikamano kisichoweza kubadilishwa katika maendeleo na kukua kwa haraka kwa mabadilishano ya kampuni mbalimbali za kimataifa mbalimbali za tasnia ya utalii zisitumie vibaya nafasi zilizonazo, ziepuke kuwa vyombo vya mifano bandia ya kiutamaduni na kijamii iliyowekwa kwenye jamii za wenyeji; ili kupata uhuru wa kuwekeza na kufanya biashara ambao hauna budi kutambuliwa kwa ukamilifu, hawana budi kujihusisha katika maendeleo ya eneo hilo, hawana budi kuepuka uhamishaji mkubwa wa faida zao au bidhaa walizoingiza kutoka nje kwa motisha, pia upunguzaji wa michango yao kwa shughuli za uchumi zilizoanzishwa;

6. Ubia na kuanzishwa kwa uhusiano usio na upendeleo kati ya kampuni ya nchi zinazotoa na zinazopokea watalii zinachangia maendeleo endelevu ya utalii na ugawaji sawa wa faida ya ukuaji wake;

## *Ibara ya 10*

Utekelezaji wa misingi ya Kanuni za Maadili ya Utalii Duniani

1. Wadau wa serikali na sekta binafsi katika uendelezaji utalii hawana budi kushirikiana katika utekelezaji wa misingi hii na kusimamia matumizi yake kikamilifu;

2. Wadau wa maendeleo ya utalii hawana budi kutambua dhima ya Asasi za Kimataifa, ambapo Shirika la Utalii Duniani ndilo la kwanza, na Asasi Zisizo za Serikali, zenye uwezo katika uga wa ukuzaji na uendelezaji utalii, ulinzi wa haki za binadamu, mazingira au afya, kwa kuheshimu misingi ya jumla ya sheria za kimataifa;

3. Wadau haohao hawana budi kuonyesha nia yao ya kufikisha migogoro yoyote inayohusu matumizi au tafsiri ya Kanuni za Maadili ya Utalii Duniani kwa ajili ya usuluhishi kwenye chombo cha tatu kisicho na upendeleo kinachojulikana kama Kamati ya Maadili ya Utalii Duniani.

**SHIRIKA LA UTALII DUNIANI**

ni shirika pekee linalojumuisha serikali mbalimbali linalohudumia dunia nzima kwa ajili ya sera na masuala ya utalii. Wanachama wake ni pamoja na nchi na maeneo 138 na wanachama shirikishi/walioshirikishwa 350 kutoka kwenye sekta za Serikali na binafsi. Jukumu la WTO ni kukuza na kuendeleza utalii kama njia muhimu ya kukuza amani na maelewano ya kimataifa, maendeleo ya kiuchumi na biashara ya kimataifa.

TOVUTI: www.world-tourism.org